*Namba ya Mtahiniwa: ……………………………………………..*

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**

**MTIHANI KABLA YA UTAMILIFU KIDATO CHA PILI MACHI 2023**

**KISWAHILI**

**MSIMBO: 021** **SIKU IJUMAA TAREHE 24/03/2023 Mchana**

---

**MUDA: MASAA 2:30**

**MAELEKEZO**

1. Mtihani huu una sehemu A,B na C
2. Jibu maswali yote kila sehemu
3. Fuata maelekezo ya kila sehemu na kila swali
4. Simu z amkononi na vifaa vyote vilivyozuiliwa havuiruhusiwi katika chumba cha mtihani
5. Majibu yote yaandikwe kwenye sehemu zilizoandaliwa
6. Andika namba yako kwenye kila kurasa upande wa juu kulia

*Namba ya Mtahiniwa: …………………………………………..*

**SEHEMU ''A" (Alama 15)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Katika kipengele (i) – (x) , chagua herufi ya jibu sahihi zaidi kisha andika herufi hiyo kwenye kijisanduku cha kujibia

i) Sifa mojawapo ya kazi ya fasaihi simulizi ni uhai. Lipi kati ya hayo si majukumu ya hadhira katika kazi ya fasihi simulizi?
A. Kuitikia kiitikio
B. Kupiga makofi kuonesha kuridhishwa
C. Kutamba kazi ya fasihi simulizi
D. Kupiga vigelegele na kushangilia

ii) Juma huimba vizuri sana. Neno lililopigiwa mstari linafanya kazi ya aina ipi ya neno?
A. Kielezi
B. Nomino
C. Kivumishi
D. Kitanzi

iii) Bainisha sentensi yenye makosa kati ya sentensi ulizopewa
A. Samata ni mchezaji hodari
B. Chai imeingia nzi
C. Paka wangu ameibiwa
D. Nyumba zilisombwa na mvua

iv) Katika mkutano wa Bunge liloisha, wabunge walisisitiza matumizi ya "Guruneti" Je maneno yaliyokolezwa wino ni rejesta ya mahali gani?
A. Bungeni
B. Mashuleni
C. Jeshini
D. hospitalini

v) Kila zamana mismu yake na kila msimu huzuka ili kukidhi haja ya mawasiliano. Je msimu **CHAKACHUA** uliibuka kipindi gani?
A. Kipindi cha mfuno wa vyama vingi vya siasa
B. Kipindi cha njaa mwaka 1979-1982
C. Enzi ya vita ya Kagera
D. Kipindi cha uhaba wa mafuata ya petrol miaka ya 2010

vi) wewe na rafiki yako mmepewa kazi ya kubainisha sentensi yenye vivumishi vya a-unganifu katika tungo . Je ni sentensi ipi kati ya zifuatazo itakuwa sahihi?
A. Kisima cha wanakijiji kimekauka maji
B. Juma na Asha wameondoka jana
C. Mwanafunzi mtoro ameadhibiwa
D. Mtoto ancheza uwanjani

vii) Sababu zifuatazo husababisha kutokea kwa utata katika tungo isipokuwa
A. Kutotamka neno ulilokusidia kwa usahihi
B. Neno kuwa na maana zaidi ya moja
C. Kuzingatia taratibu za uandishi
D. Kutumia maneno yenye maana ya picha

viii) Kati ya sababu zifuatazo ni ipi si sahihi kuhusu matumizi ya kamusi?
A. Kujifunzia lugha za kigeni
B. Kubaini kategoria ya maneno
C. Kujua tahajia z amaneo
D. Kusanifisha maneno mapya

ix) Ni methali ipi inayohusiana kimaana na methali "La kuvunda halina ubani"?
A. Maji yakimwagika hayazoleki
B. Haraka haraka haina baraka
C. Samaki mkunje angali mbichi
D. Umoja ni nguvu utengeno ni udhaifu

x) Unyambulishaji katika lugha ya Kiswahili huhusisha upatikanaji wa viambishi
A. Kabla, katikati na baad aya mzizi
B. Kabla na baada ya mzizi wa neno
C. Katikati, baada na kabla ya mzizi wa neno
D. Kabla na baada ya kiambishi.

2. Oanisha maana ya dhana zilizopo katika ORODHA ''A'' kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi iliyopo katika ORODHA ''B'' kisha andika herufi husika katika karatasi hii.

| **ORODHA ''A''** | **ORODHA ''B''** |
|---|---|
| (i) Kidahizo | A. Kamusi iliyoandikwa kwa lugha moja. |
| (ii) Sherehe ya kamusi | B. Neno linaloingizwa kwenye kamusi kwa wino uliokozwa |
| (iii) Kitomeo | C. Sehemu ya mwanzo ya kamusi |
| (iv) Kamusi thaniya | D. Kidahizo pamoja na taarifa zake zote |
| (v) Matini ya kamusi | E. Sehemu ya mwisho ya kamusi |
| | F. Fasihi au maana za maneno |
| | G. Kamusi iliyoandikwa kwa lugha mbili. |
| | H. Kiini cha kamusi |
| | I. Huandikwa kwa lugha moja na kufafanuliwa kwa lugha ziadi ya moja. |

| **i** | **ii** | **iii** | **iv** | **v** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

*Namba ya Mtahiniwa: ……………………………………………..*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**SEHEMU ''B" (Alama 70)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

3. (a) Maneno katika lugha yana dhima mbalimbali, bainisha aina ya vivumishi katika tungo zifuatazo:-
   i) Maembe yaliyoanguka yataokotwa kesho
      (a) Kivumishi________________________________________
      (b) Aina __________________________________________
   ii) Kiti kingine kipelekwe jikoni
      (a) Kivumishi________________________________________
      (b) Aina __________________________________________
   iii) Pete ya dhahabu imepotea
      (a) Kivumishi________________________________________
      (b) Aina __________________________________________
   iv) Msichana yupi anaumwa?
      (a) Kivumishi________________________________________
      (b) Aina __________________________________________
   v) Watoto wachafu wameadhibiwa vikali
      (a) Kivumishi________________________________________
      (b) Aina __________________________________________

   (b) Badili nomino zifatazo kuwa vitenzi?
   i) Kilio______________________________
   ii) Taarifa____________________________
   iii) Wimbo_____________________________
   iv) Umbo______________________________
   v) Kiima______________________________

4. Tumia mofimu zifuatazo kuonesha kazi ulizopewa katika mabano

   Mfano: Li - (wakati ulipita) - Aliondoka

   i) Ku - ( Kuonesha urejeshi wa mtendwa)

   ______________________________________________

   ii) O - (Kuonesha mzizi wa neno)

   ______________________________________________

   iii) Me - (kuonesha hali timilifu)

   ______________________________________________

   iv) Ku - ( Wakati uliopita)

   ______________________________________________

   v) M - ( Kuonesha nafsi)

_______________

vi) Ki - (Kuonesha udogo wa kitu)

_______________

vii) Ni - (kuonesha kishirikishi)

_______________

viii) Ji- (Kuonesha ukubwa wa kitu)

_______________

ix) Si - (Kuonesha ukanushi)

_______________

x) Ki – (Kuonesha hali ya masharti)

_______________

5. Watuimaji wa lugha ya Kiswahili hufanya makosa mbalimbali wakati wanapozungumza. Ukiwa kama mtaalamu bainisha makossa matano ya kisarufi na kwa kila kosa toa mfano mmoja mmoja

i) Kosa _______________
Mfano _______________

ii) Kosa _______________
Mfano _______________

iii) Kosa _______________
Mfano _______________

iv) Kosa _______________
Mfano _______________

v) Kosa _______________
Mfano _______________

6. Vijana wa kisasa hupenda sana kuzusha maneno yao ambayo wao huyatumia na pale wanapoona yamewachosha huachana nayo

(a) Kwa hoja tano onesha faida ya maneno hayo

i) _______________
ii) _______________
iii) _______________
iv) _______________
v) _______________

(b) Kwa hoja tano onesha madhara yanayoweza kuletwa kutokana na utumizi wa maneno hayo

i) _______________
ii) _______________
iii) _______________

iv) ____________________________________________________________

v) ____________________________________________________________

7. Soma kifungu cha habari kifuatacho. Kisha jibu maswali yanayofuata:

Siku zote madereva hupambana na hatari mbalimbali wanapoendesha magari yao barabarani. Hatari hizo husababishwa na ubovu wa magari, uzembe wa waenda kwa miguu na hali ya barabara yenyewe. Kusudio la Taifa siku zote ni kuwa na dereva wa kujihami, ambaye atahakikisha usalama barabarani wakati wote.

Dereva bora lazima awe na utaalamu wa kutosha katika kazi yake. Awe na mbinu kahda za kutumia katika kukwepa ajali na kujiokoa yeye, gari lake na watumiaji wengine wa barabara. Lazima uwezo wake w akujua na kutambua hatari uwe mkubwa. Asiende kwa kudhani au kuuubahatisha, bali awe na uhakika ang'amue hatari mapema na aamue kukwepa hatari na vikwazo vya barabarani.

Si hivyo tu, bali pia ajitahidi kuepuka hatari na kuzuia janga kutokea. Ajifunze na atumie mbinu mbalimbali wakati ufaao. Aendeshe kwa kufikiria mbele zaidi na akihisi tatizo atekereze maamuzi mara moja. Asingojee yatokee aepushe shari, asiwaze kuwa dereva mwenzake ndiye atasimama bali asimame yeye.

Wanafunzi wanaokwenda shuleni na wazee wamo hatarini zaidi kuliko watu wazima. Hivyo ni muhimu watu hao walindwe na wafundishwe juu ya usalama barabarani. Kwa hiyo, waendeshe vyombo vya moto wahakikishe ubora wa afya zao kabla ya kuendesha. Aidha magari yakaguliwe mara kwa mara ili yasisababishe ajali za barabarani. Tukizingatia hayo, ajali za barabarani zitapungua kama siyo kuisha kabisa

**MASWALI**

(a) Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisizidi maneno matano ______________________________________

(b) "Dereva bora ni yule anayejihami" Usemi huo una maana gani?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

(c) Usalama barabarani unamhusu nani hasa?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

(d) Taja watumiaji wawili wa barabara amabo wapo hatarini Zaidi wawapo barabrani kulingana na habari uliyosoma.

____________________________________________________________

____________________________________________________________

(e) Orodhesha hatari tatu anazokumbana nazo dereva anapokuwa barabarani.

i) ____________________

ii) ____________________

iii) ____________________

8. Kila jambo lina faida na hasara zake. Kwa kila kipengele kifuatacho eleza faida moja na hasara moja.

i) Michezo ya watoto
Faida____________________
Hasara____________________

ii) Tambiko
Faida____________________
Hasara____________________

iii) Utani
Faida____________________
Hasara____________________

iv) Majigambo
Faida____________________
Hasara____________________

v) Mivigha
Faida____________________
Hasara____________________

9. Eleza sifa tano bainifu za fasihi simulizi

i) ____________________

ii) ____________________

iii) ____________________

iv) ____________________

v) ____________________

## SEHEMU ''C" (Alama 15)

10. Wewe unaitwa Faraja Maringo na sanduku lako la barua ni 321 Mwanza. Hivi sasa unaumwa na umelazwa hospitali ya Mjini Mwanza. Andika barua kwa kaka yako anayeitwa Samweli maringo wa sanduku la posta 206 Arusha ukimjulisha jinsi hali yako inavyoendelea.

____________________

____________________

____________________

____________________